



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA**

# **TAARIFA YA SPIKA**

27 JANUARI, 2016

## **TAARIFA YA SPIKA**

Leo Jumatano tarehe 27 Januari, 2016 wakati wa kikao cha asubuhi Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Wasanii na Michezo alitoa kauli za Mawaziri inayohusu Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) Kutorusha moja kwa moja vipindi vya vikao vya Bunge kuanzia Mkutano wa pili wa Bunge.

Baada ya mawasilisho hayo, Mhe. Zitto Zuberi Kabwe (Mb) alisimama kwa kutumia kanuni ya 69(1) kutaka kutoa hoja ya kuahirisha mjadala wa hoja ya kujadili Hotuba ya Rais iliyo mbele ya Bunge tangu jana kwa majadiliano.

Mwenyekiti alimtaka Mhe. Zitto Kabwe (Mb) asome fasili ya pili (2) ya kanuni ya 69, amabayo inasomeka kama ifuatavyo:-

*"Kama Spika atakuwa na maoni kwamba kuwasilishwa kwa hoja hiyo kinyume cha uendeshaji bora wa shughuli za Bunge, atakataa kuitoa ili iamuliwe vinginevyo, papo hapo atawahoji wabunge juu ya hoja hiyo kadri atakavyoona inafaa".* Mwisho wa Kunukuu

Baada ya fasili hiyo ya 69 (2) kusomwa Mwenyekiti aliona kwamba, hoja ya kuahirisha mjadala itakuwa ni kinyume cha uendeshaji bora wa shughuli za Bunge.

Hivyo hakuitoa hoja hiyo iamuliwe na Bunge.

Msingi wa uamuzi huo wa Mwenyekiti ni kanuni ya 52(2) ya kanuni za Bunge ikisomwa pamoja na kanuni ya 53 ambayo inatamka kwamba "Baada ya Spika kutoa wito huo Mbunge yeyote

binafsi hataruhusiwa kutoa hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge wala kuuliza swali”

Baada ya mjadala kuanza Mbunge yeyote Binafsi hataruhusiwa kutoa hoja ya kuahirisha Shughuli za Bunge, hata hivyo Mwenyekiti alitoa ushauri kwa Mhe. Zitto Kabwe kwamba uamuzi huu haumzuwii kuleta hoja ya kutaka kujadili maudhui ya Kauli ya Waziri kwa utaratibu wa kawaida.

Hata hivyo wakati Mwenyekiti alipotaka kuendelea kuita wachangiaji wa Hotuba ya Rais, Mhe. Halima Mdee (MB) alisimama na kudai kwamba kauli ya Waziri inaingilia haki za Bunge hili; kwa mujibu wa Kanuni ya 51.

Jambo hili lilizua sintofahamu iliyosababisha Mwenyekiti kusitisha shughuli za Bunge ili kulifikisha suala hili kwenye Kamati ya Uongozi.

Kamati ya Uongozi imekutana chini ya mwenyekiti wake Mhe. Spika wa Bunge na baada ya kulijadili suala hili, imeamua kama ifuatavyo:-

1. Mwenyekiti wa Bunge alikuwa sahihi katika kwa uamuzi wa kukataa hoja ya kuahirisha mjadala wa Hotuba ya Rais ili kujadili kauli ya Waziri.
2. Kwa mujibu wa Kanuni ya 51 hakuna haki yoyote ya Bunge ilivunjwa kwa mujibu wa Sheria ya Haki, Kinga

na madaraka ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 51 ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

3. Hoja iliyo mbele ya Bunge ya Hotuba ya Rais, mjadala uendeleo kama ulivyopangwa kwenye Orodha ya Shughuli za leo.

---